

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE**



**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA HALMASHAURI  
KWA KUTUMIA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI( AJIRA YA MUDA) NAFASI 10**

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe anawatangazia wakazi wote wa wilaya ya Karagwe wenye sifa za kazi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za kielektroniki kuwa kuna kazi ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri katika vizuizi/belia ambayo itakuwa ni ya muda wa miezi mitatu.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

**A. SIFA ZA MSINGI**

1. Waombaji wawe Raia wa Tanzania wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
2. Elimu ya kidato cha 4 na kuendelea
3. Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai
4. Awe na uwezo wa kufanya kazi katika eneo lolote atakalopangiwa ndani ya wilaya ya Karagwe

**B. SIFA ZA ZIADA**

1. Waombaji wenye uwezo wa kutumia simu( smartphones) watapewa kipaumbele
2. Waombaji wenye uzoefu wa kukusanya mapato watapewa kipaumbele
3. Waombaji wenye mafunzo ya mgambo watapewa kipaumbele

**C. KAZI ZA KUFANYA**

1. Kukusanya mapato ya Halmashauri kwa kutumia mashine ya kielektroniki.
2. Kudhibiti myanya inayotumika kukwepa kulipa mapato ili kuongeza ukusanyaji

3. Kuhakiki stakabadhi zote zitakazopita katika eneo lako la kazi ambazo zimelipiwa katika maeneo mengine
4. Kukagua na kuhakiki mizigo ndani ya magari kabla ya kutoza ushuru ili kubaini kiasi sahihi kinachotakiwa kutozwa ushuru
5. Kuwepo muda wote katika kituo chako cha kazi kulingana na ratiba yako.
6. Waombaji wataajiriwa kwa muda.


BARUA ZA MAOMBI YA KAZI ZIANDIKWE KWA MKONO WA MWOMBAJI AKIONYESHA ANUANI KAMILI( ANAPOISHI) NA NAMBA YAKE YA SIMU PAMOJA NA KUAMBATANISHA NAKALA ZA VYETI VYOTE VYA ELIMU NA MAFUNZO PAMOJA NA WASIFU WA MWOMBAJI IKIONYESHA NA WADHAMINI WAWILI WENYE MALI ISIYOHAMISHIKA.

**NB: BARUA ZOTE ZA MAOMBI ZIPITISHWE KWA MTENDAJI WA KATA**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE  
S.L.P 20  
KARAGWE

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10 January 2020**



.....  
**GODWIN M KITONKA**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**KARAGWE**